TANGAZO LA SERIKALI NA. 436 la Tarehe 31/5/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16 (1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MANISPAA YA IRINGA MWAKA 2024

Jina

T.S Na 29 ya 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ya Mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya aya ya 12

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya aya ya 12 kama ifuatavyo:

*"Ulipaji wa gharama za kuhifadhi chombo kilichokamatwa*

"12. (1) Halmashauri itatoza kiasi cha shilingi elfu hamsini kila siku kwa chombo kilichobeba mzigo ulioshikiliwa baada ya kukamatwa ukisafirishwa bila ya kulipa ada au ushuru.

(2) Endapo chombo kilichokamatwa kitakuwa hakijalipiwa gharama za kuhifadhiwa baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya

kukiuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya mahakama na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa chombo hicho baada ya kutoa gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za mnada na gharama nyingine kama itakavyoamuliwa na Mahakama.

(3) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika aya ndogo ya (1) na (2), kabla ya kuuza chombo hicho kilichokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kukiuza".

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) kwa kufuta maneno-

(i) "Udhamini wa vipindi, filamu na tamthilia" yaliyo katika sehemu ya kumi na sita kipengele cha 16 na badala yake kuweka maneno "Tangazo la biashara linayodhamini vipindi, filamu na tamthilia katika televisheni ya Iringa".

(ii) "Taarifa ya Habari" yaliyo katika sehemu ya kumi na sita kipengele cha 17 na badala yake kuweka maneno "Tangazo la biashara wakati wa taarifa ya habari inayosomwa katika televisheni ya Iringa".

(iii) "Maandishi kupita sauti" yaliyo katika sehemu ya kumi na sita kipengele cha 18 na badala yake kuweka maneno "Tangazo la biashara la maandishi linalopita bila sauti wakati wa vipindi, filamu na tamthilia bila sauti katika

televisheni ya Iringa".
(iv) "Picha" yaliyo katika sehemu ya kumi na sita kipengele cha 19 na badala yake kuweka maneno "Tangazo la biashara la maandishi linalopita na sauti wakati wa vipindi, filamu na tamthilia bila sauti katika televisheni ya Iringa".

(v) "Picha" yaliyo katika sehemu ya kumi na sita kipengele cha 20 na badala yake kuweka maneno "Tangazo la biashara la maandishi linalopita na sauti wakati wa vipindi, filamu na tamthilia katika televisheni ya Iringa"

(vi) "Mahojiano" yaliyo katika sehemu ya kumi na sita kipengele cha 21 na badala yake kuweka maneno "Tangazo la biashara la maandishi linalopita wakati wa mahojiano bila sauti katika televisheni ya Iringa".
(vii) "Matangazo ya makampuni mbalimbali asubuhi, mchana na jioni" yaliyo katika sehemu ya kumi na sita kipengele cha 22 na badala yake kuweka maneno "Matangazo ya biashara ya makampuni mbalimbali yanayorushwa kwenye televisheni ya Iringa asubuhi, mchana na jioni".
(b) kwa kufuta Sehemu ya Kumi na Saba.

(c) kwa kubadili mpangilio wa Sehemu ya Kumi na Nane hadi Sehemu ya Ishirini na Tano na kuwa Sehemu ya Kumi na Saba hadi Sehemu ya Ishirini na Nne mtawalia.

Dodoma,
18 Aprili, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa)*